

**Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga (kushoto) akimkabidhi kitambulisho mkulima bora wa zao la korosho wakati wa ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa wadau wa korosho mkoani Lindi.** (Na Mpigapicha Wetu)

# Baraza la Veterinari laweka utambuzi kwa wafugaji

**Na Oscar Mzuka, Dodoma**

■■BARAZA la Veterinari Tanzania lilyoko chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, imeweka utambuzi rahisi kwa wafugaji ili kuwatambua vyema madaktari wa mifugo, ili kuepukana na wale vishoka.

Akizungumza na Majira Jijini Dodoma jana Msajili wa Baraza hilo, Dkt. Bedan Masuruli alisema utambuzi huo ni beji maalumu, kitambulisho na mavazi maalumu zenye lebo ya Veterinari.

Dkt. Masuruli alisema mfumo huo wa utambuzi, utawasaidia wafungaji kuepukana na vishoka na serikali kutimiza lengo lake la kuwadhibiti vishoka.

Dkt. Masuruli aliwaomba wafugaji kutoa taarifa pindi wanapokuwa na mashaka kwa vishoka wanaojitambulisha kama ni madktari, kutoa taarifa kwa baraza hilo na pia kwa Ofisi za Veterinari popote pale kuanzia ngazi za wilaya.

"Si kwamba tutafanikiwa kuwadhibiti vishoka kwa asilimia 100, lakini watapungua kwa kiwango kikubwa na sasa hivi wanafanya kazi hizo kwa kujificha, tofauti na hapo awali," alisema Dkt. Masuruli.

Dkt. Masuruli pia alivishukuru vyombo vya habari kwa jinsi vinavyoendelea kusaidia kubainishwa kwa vishoka hawa, ili kuweza kuwanusuru wafungaji kuingia katika mitego ya vishoka.

Scanned with CamScanner

> ... ...Kagera is among few regions in the country that use three means of transport simultaneously, air, lake and road



Angelah Kairuki (C), Minister of State in the Prime Minister's Office (Investment), pictured in Dar es Salaam yesterday presenting computers and various other office equipment to Salim Lueck - a representative of a group of people with impaired eyesight. The items were donated by Najal Saad (R).

THE GUARDIAN PG 4-

# DC orders police to arrest officials linked to Siha cattle thefts

By Guardian Correspondent, Siha

Speaking at Mbi Moshi village near the ranch, Mpina gave 15 days for all ...

He also instructed TALIRI to make repairs to the dip for their livestock within 15 days and the government ...



unaovutwa na ng'ombe kutokana na magari kushindwa kufika shambani kwa sababu ya ubovu wa barabara. Vijana hao walikutwa jana wakiyasogeza mazao yao sehemu wanayoweza kupata usafiri wa gari. **Picha na Said Ng'amilo**

MWANANCHI UK 22

# TADB kukabili uvuvi haramu

Mwandishi Wetu, Mwananchi

**Kilimanjaro.** Katika juhudi za kupunguza uvuvi haramu, Benki ya Kilimo Tanzania (TADB) imejipanga kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wavuvi wa Bwawa la Nyumba ya Mungu.

Mkakati huo umebainishwa na mkurugenzi mkuu wa benki hiyo, Japhet Justine baada ya kutembelea bwawa hilo kujionea shughuli zinazofanywa na wavuvi akiwa ameambatana na Waziri wa Mifugo, Luhaga Mpina.

"Kumekuwa na matumizi ya zana zisizo na ubora hali inayopunguza maalia ya samaki na kuzorotesha mapato katika sekta hii. TADB tunatoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wavuvi ili kuwa na uvuvi endelevu kote nchini," alisema Justine.

Aliongeza kuwa milango ipo wazi kwa benki na taasisi za fedha kushirikiana na TADB kupunguza changamoto zinazoikabili sekta ya uvuvi na ufugaji ambazo zimeajiri Watanzania wengi.

"Tunashirikiana na benki washirika kukabiliana na changamoto za wakulima, wafugaji na wavuvi ili kuwainua kiuchumi na kuongeza mchango wao katika uchumi wa nchi," aliongeza.

Waziri Mpina alipongeza hatua za TADB na kuwataka wavuvi kutumia vyema mikopo wanayochukua kujiletea maendeleo.

"Rasilimali za uvuvi zinatakiwa kulindwa na kila mwananchi, tunaipongeza TADB kwa kuwawezesha wavuvi kuondokana na matumizi ya zana hafifu zinazopunguza mazalia ya samaki," alisema Mpina.

Mbali na zana za kisasa kwa wavuvi, alisema wizara itashirikiana na Jeshi la Polisi pamoja na Halmashauri ya Mwanga kuendesha operesheni maalumu ya kupambana na uvuvi haramu.

"Hizi zote ni hatua za kuwasaidia wavuvi, tutachoma nyavu zote zisizokidhi viwango," alisema Waziri Mpina.

**SOKO LA UVUVI**

# Rukwa kusindika samaki

**20**

**Tani ambazo kiwanda cha Alpha Tanganyika Flavour kinaweza kusindika kwa siku.**

**100**

**Wafanyakazi watakaoajiriwa k**

Mwandishi Wetu, Mwananchi

**Sumbawanga.** Ili kutoa soko la uhakika kwa wavuvi waliopo na kukuza kipato cha kaya na halmashauri, Mkoa wa Rukwa umejenga kiwanda cha kusindika samaki kitakachoanza uzalishaji mwezi ujao.

Mradi huo unaosimamiwa na kampuni ya Alpha Tanganyika Flavour kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni utekelezaji wa agizo la Rais John Magufuli alilolitoa mwaka jana alipofanya ziara mkoani hapa.

Rais aliagiza wizara hiyo kuhakikisha kiwanda cha kusindika samaki kinaanzishwa mkoani hapa ili kutoa soko la uhakika kwa wavuvi waliopo.

Kutekeleza hilo, Alpha Tanganyika Flavour kwa kushirikiana na wizara wamekarabati kiwanda kilichokuwepo ili kuanza kusindika samaki hivi punde.

Katibu mkuu wa Uvuvi, Dk Rashid Tamatamah alitembelea kiwanda hicho jana kukagua maendeleo ya ukarabati unaofanywa mjini Sumbawanga.

"Leo nimekuja na wataalamu wangu kukagua ukarabati unaoendelea, ukikamilika kiwanda kitatoa ajira 100 kwa wananchi na hivyo kuongeza mapato ya Serikali," alisema Dk Tamatamah.

Kwa uwezo wake, kiwanda hicho kinaweza kusindika tani 20 za samaki kwa siku ambazo zinakidhi vigezo vya kuuzwa katika masoko ya ndani na nje hasa Marekani na Ulaya.

Dk Tamatamah alimpongeza mkurugenzi mtendaji wa Alpha Tanganyika Flavour, Alpha Nondo kwa kufanya uwekezaji huo kwamba ni mfano wa ushirikiano wa sekta binafsi na Serikali.

Kwa upande wake, Nondo aliishukuru Serikali kwa ushirikiano inaompatia na kusema kiwanda hicho kitatoa majibu ya kero za wavuvi waliokuwa wanahangaika kutafuta soko la samaki huku kikitekeleza agizo la Rais magufuli.

"Kiwanda cha Alpha kitamkomboa mvuvi aliyekosa uhakika na soko la samaki wake. Nawaomba wavuvi na wananchi kutupa ushirikiano ili kiwanda kiwahudumie vizuri," alisema Nondo.

Katibu tawala msaidizi wa Mkoa wa Rukwa, Oerani Chengula alisema kwa muda mrefu walikuwa wanahangaika kupata kiwanda cha kusindika samaki wanaovuliwa mkoani hapa.

"Tunaamini kuanzishwa kwa kiwanda hiki kutatoa ajira kwa watu wetu na kitatuongezea mapato ya halmashauri. Wavuvi wataacha uuzaji holela wa samaki wao kwa sababu soko la uhakika litakuwa limepatikana kupitia kiwanda hiki," alisema

Scanned with CamScanner

UHURU UK 8

**Tuhuma>> Wizi wa ng'ombe 17 mali ya serikali**

# DC Siha aagiza watumishi wote West Kilimanjaro wakamatwe

**Na MWANDISHI WETU,** Siha

MKUU wa Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, Onesmo Buswelu, ameagiza jeshi la Polisi kuwakamata watumishi wote wa Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) West Kilimanjaro, kufuatia kashfa ya kupotea kwenye Mazingira ya kutatanisha ng'ombe 17 wa serikali waliokuwa wanatunzwa kwenye ranchi hiyo.

Buswelu, amesema tangu wizi huo ulipofanyika, hakuna taarifa yoyote iliyowasilishwa kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama ya wilaya hiyo, jambo linaonesha kuna njama za makusudi zilizofanywa na watumishi hao kuibia serikali, jambo ambalo halikubaliki.

Mkuu huyo wa wilaya alitangaza uamuzi huo mwishoni mwa wiki iliyopita, baada ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, kutembelea Ranchi ya West Kilimanjaro na kupokea taarifa ya kuwepo wizi wa ng'ombe hao wa serikali huku kukiwa hakuna hatua zozote zilizochukuliwa dhidi ya watumishi waliohusika na wizi huo.

Akizungumza na watumishi wa Ranchi ya West Kilimanjaro, Waziri Mpina, alieleza kutoridhishwa na hatua zilizochukuliwa na uongozi kuhusiana na kashfa hiyo na kuagiza ifikapo Agosti 19, mwaka huu mifugo yote iliyopotea iwe imerejeshwa ndani ya ranchi hiyo.

Mpina alisema hatua zilizochukuliwa za kuwasimamisha kazi watumishi wawili kufuatia wizi huo, ni njama za kuficha mtandao wa uhalifu huo na kuagiza vyombo vya dola kufanya uchunguzi wa kina ili kuunasa mtandao wote uliohusika katika kashfa hiyo.

Alimuagiza Meneja Mkuu wa NARCO, kuwasimamia kikamilifu watumishi wake katika ulinzi wa rasilimali hizo za nchi na kutokuwa sehemu ya kuhujumu na kushiriki vitendo vya wizi.

Akizungumza kwenye mkutano uliofanyika Kijiji cha Miti Mirefu, kinachopakana na Ranchi ya West Kilimanjaro pamoja na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo West Kilimanjaro, Waziri Mpina, alitoa siku 15, kwa wafugaji waliopangisha kwenye maeneo ya TALIRI, kulipa deni la sh. milioni 19, walioshindwa kufanya hivyo, serikali itavunja mikataba na kuwaondoa kwenye hilo.

Pia ameagiza TALIRI ndani ya siku 15, iwe imekarabati josho na wananchi waanze kuogesha mifugo yao na serikali itapeleka dawa ya ruzuku huku akiagiza NARCO, kukarabati majengo ya TALIRI ili yatumiwe na wananchi hao kama zahanati na kumuagiza Mkurugenzi wa Wilaya ya Siha, kuhakikisha anapeleka daktari na dawa.

Kuhusu malalamiko ya wafugaji ya kukosa njia ya kupitisha mifugo kwenda kunywa maji, amemuagiza Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi wa Halmashauri, kushirikiana na wananchi na wawekezaji kutengeneza njia ya mifugo ili wafugaji hao kumaliza mgogoro huo.

Waziri Mpina, alisema serikali inaendelea kuboresha maisha ya wafugaji, ndio maana imetengeneza kanuni mpya, zikiwemo za chanjo ili kulinda mifugo kwa magonjwa na kuweka bei elekezi za chanjo, ambazo zitashuka kwa asilimia 60, hivyo wafugaji watagharamia asilimia 40, yakiwa matunda ya serikali ya Dk. John Magufuli.

**MSAADA**



# Watumishi NARCO matatani tuhuma upotevu wa ng'ombe

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

MKUU wa Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, Onesmo Buswelu, ameagiza Jeshi la Polisi kuwakamata watumishi wote wa Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) West Kilimanjaro kufuatia kashfa ya kupotea kwenye mazingira ya kutatanisha ng'ombe 17 wa serikali waliokuwa wanatunzwa kwenye ranchi hiyo.

Buswelu amesema tangu wizi huo ufanywe, hakuna taarifa yoyote iliyowasilishwa kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya hiyo, jambo linaonyesha kuna njama za makusudi zilizowekwa na watumishi hao kuiba serikali.

Alitoa uamuzi huo jana baada ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, kutembelea Ranchi ya West Kilimanjaro na kupokea taarifa ya kutoweka wizi wa ng'ombe hao wa serikali, huku kukiwa hakuna hatua zozote zilizochukuliwa dhidi ya watumishi waliohusika na wizi huo.

Akizungumza na watumishi wa ranchi hiyo, Waziri Mpina alieleza kutoridhishwa na hatua zilizochukuliwa na uongozi wa ranchi kuhusiana na kashfa hiyo na kuagiza kuwa ifikapo Jumatano (kesho), mifugo yote iliyopotea iwe imerejeshwa ndani ya ranchi hiyo. Waziri Mpina alisema hatua zilizochukuliwa za kuwasimamisha kazi watumishi wawili kufuatia wizi huo ni njama za kuficha mtandao wa uhalifu huo na kuagiza vyombo vya dola kufanya uchunguzi wa kina ili kunasa mtandao wote uliohusika katika kashfa hiyo.

Alimwagiza Meneja Mkuu wa NARCO kuwasimamia kikamilifu watumishi wake kusimamia ulinzi wa rasilimali hizo za nchi na kutokuwa sehemu ya kuhujumu na kushiriki vitendo vya wizi.

Akizungumza kwenye mkutano uliofanyika Kijiji cha Miti Mirefu kinachopakana na Ranchi ya West Kilimanjaro pamoja na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo West Kilimanjaro, Waziri Mpina alitoa siku 15 kwa wafugaji waliopangisha kwenye maeneo ya (Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI), kulipa deni la Sh. milioni 19 na wakishindwa kufanya hivyo, serikali itavunja mkataba na kuwaondoa kwenye hilo.

Pia, aliagiza TALIRI kuhakikisha ndani ya siku 15 iwe imekarabati josho na wananchi na waanze kuogesha mifugo yao na serikali itapeleka dawa ya ruzuku, huku akiagiza NARCO kukarabati majengo ya TALIRI ili yatumiwe na wananchi hao kama zahanati.

Kufuatia malalamiko ya wafugaji ya kukosa njia ya kupitisha mifugo, Waziri Mpina alimwagiza Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi wa Halmashauri kwa kushirikiana na wananchi na wawekezaji kutengeneza njia ya mifugo ili wafugaji hao kumaliza mgogoro huo.

Alisema serikali inaendelea kuboresha maisha ya wafugaji ndiyo maana imetengeneza kanuni mpya zikiwamo za chanjo ili kulinda mifugo kwa magonjwa na kuweka bei elekezi za chanjo.

Scanned with CamScanner

tiwa

ni

bainisha kuwa katika
na changamoto kadhaa
bili wakulima, ikiwemo
ika rasmi kwenye taasisi
tayari serikali imeanza
bulisho maalumu
atambulisha hususani
ji huduma za kifedha.
ulisho hivyo vya
uwa na 'chip' maalumu
i taarifa zote muhimu
ulima, hatua ambayo
tarahisishia taasisi za
ongo mrefu wa kuku-
a za wadau hao na
apatia mikopo kwa
sema Hasunga, ambaye
tano huo alikabidhi
ho hivyo vya mfano kwa
15 wa awali.
pia kwa sasa serikali
ini upya sera ya masoko
ala zima la kilimo cha
i wakulima wetu waweze
a bidhaa zao mapema,"




a ya

# Mpina akikaba koo kiwanda cha dawa za mifugo

**Na John Mhala, Arusha**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina amekiagiza kiwanda cha kuzalisha dawa za mifugo, viuatilifu na vifungashio cha Farm Access Ltd, kuongeza uzalishaji kutoka asilimia 20 ya sasa hadi asilimia 100 ili kukidhi mahitaji ya mifugo nchini.

Alitoa agizo hilo jana alipotembelea kiwanda hicho kilichopo Ngaramtoni jijini Arusha na kuwekewa jiwe la msingi katika jengo jipya la uzalishaji.

Alisisitiza kuwa iwapo kiwanda hicho kitakidhi malengo ya asilimia 100, kitaisaidia serikali kupunguza gharama kubwa za uagizaji wa dawa za mifugo nje ya nchi.

"Kwa kuwa mmeeleza wenyewe kuwa soko la bidhaa zenu ni kubwa, ni lazima muongeze uzalishaji kutoka asilimia 20 na kufikia asilimia 100 na muweze kusambaza hizi dawa maeneo mengi hapa chini," alisema.

Awali Mkurugenzi wa Biashara wa Kiwanda cha Farm Access, Danny Ngowi alisema kiwanda hicho kilianzishwa mwaka 2013 kwa lengo la kuagiza na kusambaza dawa za mifugo kutoka nje ya nchi.

Kutokana na changamoto ya baadhi ya dawa kutokuwa na ubora, wameamua kutengeneza dawa hizo zikiwa na ubora wa kiwango cha juu.

Alisema kiwanda hicho kimekuwa cha kwanza kutengeneza na kusambaza dawa za mifugo na viuatilifu kwa ajili ya soko la ndani na hiyo ni mwitikio wa sera ya serikali ya uanzishaji wa viwanda.

Alisema wakati wanaanzisha kiwanda hicho, walipata changamoto ya mitaji kutoka taasisi za fedha.

Lakini, baadaye benki mbalimbali zilionesha nia ya kutoa fedha za mikopo [illegible]

UK 21, tarehe 18/08/2020

# TADB yaguswa na uvuvi haramu bwawa la nyumba ya Mungu

**Na Mwandishi Wetu, Kilimanjaro**

MKURUGENZI Mtendaji wa Benki ya Kilimo (TADB), Japhet Justine amemhakikishia Waziri wa Mifugo na Uvuvi,Luhaga Mpina mikopo ya masharti nafuu kwa wavuvi hususani wa Bwawa la Nyumba ya Mungu ili kuondokana na uvuvi haramu.

Akizungumza na Waandishi wa Habari katika ziara ya alipotembelea bwawa la Mungu na kujionea shughuli zinazofanywa na wavuvi akiwa na Waziri wa mifugo,Mpina, Mkurugenzi Mtendaji wa TADB,Justine alisema kuwa benki hiyo imedhamiria kuleta mageuzi makubwa katika sekta ya uvuvi kwa kuwawezesha wavuvi zana za kisasa.

"Kumekuwa na matumizi ya zana zisizo na ubora katika shughuli za uvuvi hali ambayo imepelekea mazalia ya samaki kupungua na kuzorotesha mapato katika sekta hiyo. TADB tutaendelea kuunga mkono juhudi za serikali kwa kuwapa mikopo yenye masharti nafuu wavuvi ili kuwa na uvuvi endelevu kote nchini," alisema.

Justine alisema kuwa milango ipo wazi kwa mabenki na taasisi za fedha kushirikiana na Benki ya kilimo ili kupunguza changamoto zinazoikabili sekta ya uvuvi na ufugaji ambazo zimeajiri watanzania wengi.

"Tumekuwa na ushirikiano na mabenki washirika katika kuhakikisha changamoto za wakulima, wafugaji na wavuvi zinapatiwa ufumbuzi ili waweze kujinua kiuchumi na kuwafanya wachangie pakubwa katika uchumi wa nchi," alisema.

Waziri Mpina alipongeza hatua zinazochukuliwa na TADB na kuwataka wavuvi kutumia vyema mikopo inayotolewa na benki hiyo ili kuleta maendeleo ya kweli hapa nchini.

"Rasilimali za uvuvi zinatakiwa kulindwa na kila mwananchi, tunaipongeza TADB kwa uzalendo wao wa kuwawezesha wavuvi ili waweze kuondokana na uvuvi wa kutumia zana haifu ambazo zimeleta athari hasi katika sekta hii kwa kupunguza mazalia ya samaki," alisema.

Alisema kuwa mbali ya hatua zinazochukuliwa na TADB za kuhakikisha wavuvi wanakuwa na zana za kisasa, Wizara yake itashirikiana na jeshi la polisi pamoja na halmashauri ya wilaya ya Mwanga katika kutekeleza operesheni maalum ya kupambana na uvuvi haramu.

"Hatua za kuwasaidia wavuvi kwa kuwapa mikopo ya masharti nafuu kutoka benki ya maendeleo ya kilimo, zipo jitihada za kuchukua ili kutokomeza uvuvi haramu ikiwemo kuchoma moto nyavu ambazo hazikidhi viwango pamoja na kuwachukulia hatua za kisheria wahusika wote ambao wamekuwa wakifanya uvuvi haramu," alisema Waziri Mpina.

Aidha Waziri Mpina alisema kuwa wavuvi wataendelea kusikilizwa na kuwataka wataalam wa wizara hiyo kuweka mikakati ambayo itawafanya wavuvi waendelee kunufaika na rasilimali hizo.

"Tunapoelekea uchumi wa viwanda lazima kufanya mageuzi katika kila sekta ikiwemo hii ya uvuvi, tutaendelea kukutana na wataalam wa wizara pamoja na wadau wa sekta ya uvuvi ili waje na mipango ya uvuvi endelevu hali ambayo itachangia ukuaji wa pato la nchi na la mwananchi mmoja mmoja," aliongeza.